

# HALMASHAURI YA KIJIJI CHA MWANAMBAYA



**UTHIBITISHO WA MAUZIANO YA ENEO LA SHAMBA/XIWANJA/NYUMBA KATIKA KITONGOJI CHA** MAAOAO

**Mimi/Sisi** KASSIM ALLI MTOPWANI

**Kwa ridhaa yangu /yetu nikiwa / tukiwa na akili timamu, bila kushawishiwa na mtu yeyote, Leo tarehe** 04-10-2023 **nimeamua/tumeamua kuuza** ENEO

**Lenye/Chenye/Yenye ukubwa wa** EKARI 3.42 **Namuuzia/tunamuuzia** MWANGAMKALI COMPANY LIMITED

**kwa thamani ya shilingi** MILLIONI TISINI TU (90,000,000/=)

**Mnunuzi amelipa shilingi** MILLIONI TISINI TU (90,000,000/=)

**Ndani ya eneo kuna** NYUMBA MBILI (2), MIEMBE NA MINAZI

**Eneo ni kwa ajili ya** UWEKEZAJI

**MIPAKA YA ENEO:**

1. **KASKAZINI:** BARABARA
2. **KUSINI:** HUSSEIN SINDA
3. **MASHARIKI:** HARUNA EMBE
4. **MAGHARIBI:** MR. YEKINI

**MASHAHIDI UPANDE WA MUUZAJI:**

1. **JINA:** RICHARD JEREMIAS MANGOSONGO **SAINI** ……… **NA** 0713624838
2. **JINA:** GRACE MISANA GAMBA **SAINI** ……… **NA** 0655133111

**MASHAHIDI UPANDE WA MNUNUZI:**

1. **JINA:** JOHN . E. MPONELA **SAINI** ……… **NA** 0784380143
2. **JINA:** ……… **SAINI** ……… **NA** ………

**JINA LA MUUZAJI / WAUZAJI**

1. **JINA:** KASSIM ALLI MTOPWANI **SAINI** ……… **NA** 0656658402
2. **JINA:** ……… **SAINI** ……… **NA** ………

**JINA LA MNUNUZI / WANUNUZI**

1. **JINA:** MWANGAMKALI COMPANY LTD **SAINI** ……… **NA** ………
2. **JINA:** ……… **SAINI** ……… **NA** ………

**Mauziano haya yamefanyika mbele ya M/kiti wa Kitongoji cha** MAAOAO

**Jina** ELIAS .A. MHAWI **Saini na mhuri** ………

**YAMETHIBITISHWA KATIKA OFISI YA KIJIJI NA:-**

1. **Mwenyekiti Wa Kijiji** LEILA .Y. CHABRUMA **Saini/Mhuri** ………
2. **Afisa Mtendaji wa Kijiji** JUMANNE .S. SHABANI **Saini/Mhuri** ………

**NB: (i) Hakikisha eneo lako linafanyiwa usafi na kutunza vyanzo vya maji kwa kuacha mita 30 kila upande.**

**(ii) Huruhusiwi kuanza ujenzi wowote mpaka upate kibali kutoka Halmashauri ya Wilaya.**

# MKATABA WA MAUZIANO YA SHAMBA / ENEO

**MKATABA HUU** wa mauziano ya shamba/eneo umefungwa leo hii tarehe **04** mwezi **Octoba, 2023**

**KATI YA**

**KASSIM ALLI MTOPWANI** wa Kijiji cha Mwanambaya katika Kitongoji cha Madodo-Mkuranga (Ambaye katika mkataba huu atajulikana kama **"MUUZAJI"** tafsiri ambayo pale inapobidi itawahusisha warithi wake kwa upande wa kwanza)

**NA**

**MKURUGENZI MTENDAJI** wa **KAMPUNI YA MWANGAMKALI** ya Jijini Dar es Salaam (Ambaye katika mkataba huu atajulikana kama **"MNUNUZI"** tafsiri ambayo pale inapobidi itawahusisha warithi wake kwa upande wa pili).

**KWA KUWA**

a. Muuzaji ndiye mmiliki wa shamba / eneo hilo lililopo katika Kitongoji cha **MADODO**, katika Kijiji cha **MWANAMBAYA**- Wilaya ya Mkuranga katika Mkoa wa Pwani.

b. Shamba / eneo lina ukubwa wa ekari 3.42 likiwa limepakana na barabara upande wa Kaskazini, upande wa Kusini linapakana na **HUSSEIN SINDA**, upande wa Mashariki linapakana na **HARUNA EMBE** na upande wa Magharibi linapakana na Bwana **YEKINI.**

c. Ndani ya shamba kuna nyumba mbili, miti ya miembe 2 na miti ya minazi kadhaa.

**d.** Uongozi wa Kijiji cha **Mwanambaya** kupitia kwa Mtendaji wa Kijiji ndugu **J.S. SHABANI** umethibtisha kuwa **KASSIM ALLI MTOPWANI** ndiye mmiliki halali wa shamba/eneo hilo alilolirithi kutoka kwa Baba yake **ALLY MOHAMEDI MTOPWANI.**

e. Muuzaji akiwa na akili zake timamu bila ya kushurutishwa na kwa hiari yake mwenyewe ana madhumuni ya kuuza shamba / eneo hilo kwa Mnunuzi kwa kuzingaria masharti yaliyoainsihwa ndani ya Mkataba huu.

f. Mnunuzi ana nia na amekubali kununua shamba/eneo hilo lililotajwa hapo juu katika aya "A" kwa gharama iliyotajwa aya ya kwanza (1) hapa chini.

**HIVYO BASI MKATABA HUU UNASHUHUDIWA NA KUFUNGWA KAMA IFUATAVYO.**

1. Muuzaji kwa hiari yake mwenyewe bila ya kushurutishwa na kwa akili zake timamu ameamua kumuuzia Mnunuzi shamba/eneo lake lililotajwa hapo juu kwa jumla ya shilingi za **Kitanzania Milioni Tisini tu (Tshs 90,000,000/=).**

2. Kwamba Mnunuzi amelipa na Muuzaji anakiri kupokea kiasi cha shilingi za **Kitanzania Milioni Tisini tu (Tshs 90,000,000/=)** fedha ambayo imewekwa na Mnunuzi katika akaunti ya Benki namba 20702501213 NMB Tawi la TEMEKE kwa maelekezo ya Muuzaji kama malipo ya Ununuzi wa shamba/eneo hilo lililotajwa kwenye mkataba huu, kwa wahusika wote kutia sahihi zao katika mkataba huu.

3. Kwamba Muuzaji anashuhudia kuwa yeye ndiye Mmiliki halali wa shamba/eneo hilo na ya kwamba hakuna pingamizi lolote wala rehani au zuio lolote la Kisheria na endapo itabainika kwamba Muuzaji hana miliki halali, basi mkataba huu utakuwa batili na Muuzaji atawajibika kumrudishia Mnunuzi fedha yote aliyoitoa chini ya mkataba huu.

4. Muuzaji na Mnunuzi wamekubaliana kwamba endapo kutakokea mabishano baina yao juu ya masharti na tafsiri ya mkataba huu; juhudi zitafanyika kutatua mgogoro huo kwa njia ya maelewano kwa kutumia Wakili/Msuluhishi watakaye mchagua kwa pamoja na endapo itashindikana kupata suluhu; wahusika watakuwa na hiari ya kwenda mahakamani.

5. Mara baada ya kutia sahihi mkataba huu, Muuzaji atamkabidhi Mnunuzi Hati na nyaraka zote zinazohusiana na Shamba/Eneo.

6. Baada ya malipo hayo; Mnunuzi anakuwa Mmiliki halali wa Shamba/Eneo hilo na Muuzaji anakubali kumkabidhi Mnunuzi Shamba/Eneo hilo na anatamka wazi kwamba kuanzia sasa Shamba/Eneo hilo siyo mali yake tena.

7. Mnunuzi amekwisha kagua Shamba/Eneo hilo na ameridhia na kukubali kwamba baada ya kufanya malipo hayo amepokea miliki rasmi ya Shamba/Eneo alilolinunua pamoja na nyaraka zote zinazohusiana na Shamba/Eneo hilo.

8. Muuzaji anatamka kwamba baada ya malipo kukamilika na Mnunuzi kukabidhiwa Shamba/Eneo alilolinunua, Muuzaji atafanya bidii kuondoka katika Shamba/Eneo hilo katika muda wa ...SIKU 7... toka kutia sahihi mauziano haya.

9. Mkataba huu utatawaliwa na kuongozwa na Sheria za Tanzania.

**KWA USHUHUDA HUU,** Pande zote husika zimekubaliana kuweka sahihi Mkataba huu katika siku na mwaka ulioandikwa hapo juu.

Imetiwa saini na **KASSIM ALLI MTOPWANI**)
ambaye namjua/ametambulishwa kwangu)
na ..........................................ambaye )
namjua leo hii tarehe.04.mwezi ./10.2023 )

.......................................
**MUUZAJI**



JOHN ESAU MPONELA ADVOCATE NOTARY PUBLIC & COMMISSIONER FOR OATHS P.O.Box 10669, D'SALAAM

**SHAHIDI WA MUUZAJI**
JINA: .RICHARD JEREMIAS MANGOSONGA.
SAHIHI..........................................
ANUANI:...TEMEKE YOMBO DSM.
.........................................

**IMETIWA** saini na **MINGYUE XIAO** )
Mkurugenzi wa Kampuni ya Mwangamkali)
ambaye namjua/ametambulishwa kwangu)
na ..........................................ambaye)
namjua leo hii tarehe 04mwezi ./10 2023 )

.......................................
**MNUNUZI**



COMMISSIONER FOR OATHS P.O.Box 10669, D'SALAAM

**SHAHIDI WA MNUNUZI**

JINA: .XU.QING.JIANG.........................
SAHIHI:..徐青江..............................
ANUANI:.........DAR ES SALAAM
.........................................

**SHAHIDI WA PANDE ZOTE MBILI**

JINA: ELIAS A. MHAWI

SAHIHI: [signature]

ANUANI: MWANAMBAYA.
MABOKO

CHEO: M/KITI KITONGOJI

**MAKUBALIANO HAYA YAMEFUNGWA NA PANDE ZOTE MBILI PAMOJA NA MASHAHIDI WAO KUTIA SAHIHI ZAO LEO HII TAREHE........ OCTOBA, 2023.**

**MBELE YANGU**

JINA: JOHN E. MPONELA

SAHIHI: [signature]

ANUANI: S.L.P. 10669
DAR ES SALAAM

JOHN ESAU MPONELA ADVOCATE NOTARY PUBLIC & COMMISSIONER FOR OATHS P.O.Box 10669, D'SALAAM

CHEO: **KAMISHNA WA VIAPO**